# TAMKO KULAANI VITENDO VYA UKATILI DHIDI YA WANAWAKE WAGOMBEA KATIKA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2020

Sisi Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu tumekuwa tukifuatilia kwa ukaribu mchakato mzima wa Uchaguzi Mkuu wa Kiti cha Urais, Ubunge na Udiwani wa Mwaka 2020. Kama wadau wa uchaguzi huu, tunasikitishwa na vitendo vya Ukatili dhidi ya Wanawake wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi vinavyoendelea kufanywa na baadhi ya wanaume wagombea au mashabiki wa wagombea wa nafasi za urais, ubunge, na udiwani pamoja na Vyombo vya Dola katika kipindi hiki cha Uchaguzi Mkuu. Kwa masikitiko makubwa tunashuhudia Ukiukwaji Mkubwa wa Haki za Wanawake wagombea nafasi hizo Kupigwa, Kuchaniwa nguo, Kutukanwa, kudhalilishwa kwa utu wao aidha kulingana na rangi au umbile la mwanamke .

Tunasikitishwa zaidi kwamba pamoja na ukiukwaji huo mkubwa wa haki za wanawake, vyombo husika vya kusimamia uchaguzi ikiwemo Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Tume ya Uchaguzi Zanzibar pamoja na Ofisi ya Msajili wa vyama Vya siasa kutochukua hatua zozote dhidi ya wahusika wa vitendo hivi vya kinyama na udhalilishaji dhidi ya Wanawake wagombea wa nafasi hizi za uongozi.

Pamoja na Jitihada zote zinazofanywa na wadau wa uchaguzi kuhakikisha wanawake wanashiriki kikamilifu na kupata nafasi za za juu za uongozi katika vyombo vya maamuzi ili kuleta usawa wa kijinsia na maendeleo endelevu. Kinyume chake jitihada hizi zinazimwa na vitendo hivi vya kikatili na kinyama vinavyoendelea kufanyika kwa uwazi na majigambo bila hatua stahiki kuchukuliwa kwa mujibu wa Sheria za Vyama vya Siasa iliyofanyiwa Marekebisho Mwaka 2019.

"….***Udhalilishaji mkubwa alioufanya Katambi Kwangu na Wanawake wote duniani………mimi ni mwanamke hivyo nikiwa kwenye Hedhi sitaweza kuwatumikia wananchi…….***" Hii ni nukuu ya Salome Makamba, Mgombea ubunge jimbo la Shinyanga Mjini kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) akilalamika kufanyiwa udhalilishaji na Patrobas Katambi, mgombea ubunge wa jimbo hilo kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM). Mfano mwingine ni wa kudhalilishwa kwa Mgombea Ubunge Jimbo la Serengeti kupitia chama Cha CHADEMA, Catherine Ruge aliyepigwa na polisi. Mgombea

ubunge jimbo la Tarime Mjini kupitia CHADEMA, Esther Matiko pia amepitia ukatili kwa walinzi kupigwa na kukamatwa mbele.

Sisi Wanawake Watetezi wa Haki za Buinadamu hapa nchini tunalaani na kukemea kuwepo na vitendo hivi vya kuwapiga na kuwadhalilisha wanawake wote wagombea wa nafasi za urais, ubunge na udiwani kwa nia ya kuwakatisha tamaa na kurudisha nyuma jitihada za kuwakomboa wanawake kushika nyazifa katika ngazi za maamuzi. Wanawake wana Haki ya kuongoza kama ilivyo kwa wanaume. Ikumbukwe kuwa nchi yetu ni huru na inafuata misingi ya haki za binadamu kama ilivyokubaliana na mataifa mengine kulinda na kutetea Haki za Binadamu kupitia mikataba mbalimbali ya kimataifa, Kikanda na Pamoja na sheria za nchi zinazolinda haki za Binadamu hususani Haki za Wanawake.

Tanzania Nchi yetu imeridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa mwaka 1966. Mkataba wa Banjul wa Afrika juu ya Haki za Binadamu na Mkataba wa Roma ulioanzisha Mahakama ya Kimataifa ya Jinai (ICC) na mngine mingi. Mikataba hii inaitaka nchi wanachama kufanya jitihada za makusudi kwa mujibu wa sheria na taratibu za kiuongozi kuhakikisha zinatoa haki kwa raia, hususani haki ya ulinzi wa utu wa mtu, haki ya kufuata utaratibu wa kisheria (due process), haki ya uhuru dhidi ya utoaji adhabu ya mateso na kutweza utu wa binadamu kijinsia, kidini au rangi yake. Zaidi, kwa mujibu wa Mkataba wa Roma, uvunjifu wa haki hizi, hususani haki ya kutumia nguvu dhidi ya raia ni sehemu ya uhalifu dhidi ya ubinadamu (crime against humanity). Pamoja na mikataba hii, pia kuna mikataba mahususi inayolinda haki za wanawake. Mathalani Mkataba wa Jinsia na Maendeleo Afrika wa Nchi za Kusini mwa Afrika, Maputo Protoko na Mkataba wa Kutokomeza Aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW). Nchi yetu pia imekuwa kinara wa kusimamia maazimio ya Tamko la Beijing.

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 14 na 15 inaeleza kuwa “Kila mtu anayo haki ya kukusanyika kwa uhuru na amani na kujumuika”. Katiba inaelekeza zaidi kuwa "Kila mtu ana haki ya kuishi na ulinzi wa maisha yake kwa mujibu wa sheria." Zaidi ya haki, Katiba inaelekeza kuwa "Kila mtu anastahili kuheshimu na kulindwa utu wake", na kwamba serikali " kuweka taratibu za kisheria kuhusu hali, njia na kiwango ambacho haki ya usalama wa mtu inaweza kuingiliwa bila kuathiri masharti ya katiba. Vyombo vya dola vina wajibu wa kulinda raia na pia kuchukua hatua stahiki pale kunapokuwa na uvunjifu wa amani.

Aidha tunatambua maelekezo ya Sheria ya Polisi na Nguvu ya Ziada, Sura 322, juu ya matumizi ya nguvu dhidi ya raia. Sheria hizi zimeelekeza hatua za kufuatwa, mathalani onyo kutolewa, na kama kuna ulazima huo na lengo kuwa kumuweka mtuhumiwa chini ya ulinzi, sio kupiga, kutesa au kutweza utu wake baada ya kumkamata. Hivi karibuni tumeshuhudia nguvu kubwa inayotumika kufifisha haki ya Wanawake kushiriki katika uchaguzi. Tunashuhudia jinsi wanawake wagombea wa nafasi za uongozi wa kisiasa kutoka vyama vyote wanavyodhalilishwa na pia nguvu kubwa sana inayotumika ambayo ni kinyume na Utawala wa Sheria na Haki za Binadamu. Tabia za kuendelea kupiga, kuwatolea lugha chafu zenye maneno ya udhalilishaji na kuwabugudhi wanawake wagombea ni njia ya kujaribu kuwatoa ili wasishiriki ipasavyo katika vinyang'anyiro hivi ni ukatili wa haki za wanawake. Aidha vitendo hivi vya udhalilishaji vinajenga hofu kwa wanawake kujitokeza kwenda kupiga kura na kushiriki katika ngazi za maamuzi na uongozi.

Sisi Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu tunatoa rai kwa vyombo vinavyosimaia uchaguzi husussani Tume za Uchaguzi Tanzania Bara na Zanzibar pamoja na Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya siasa kuchukua hatua kali za kisheria kwa mtu/watu wote waliofanya na wanaofanya vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake wagombea na wanaoshiriki katika kampeni za uchaguzi kama ilivyoelekezwa katka Sheria ya Vyama vya Siasa iliyofanyiwa marekebisho Mwaka 2019 ambayo inakataza ukatili wa aina yoyote dhidi ya wanawake. Tunazisihi mamlaka hizo kuchukua hatua zinazofaa kwa mujibu wa Sheria ili kuepusha vitendo vya vurugu, kutumia nguvu, matumizi ya lugha za matusi, kashfa, uchochezi au vitendo vingine vyovyote vinavyoweza kusababisha uvunjifu wa amani kama ilivyoelekezwa katika Kifungu cha 9(2)(f))).

Tunalitaka jeshi la polisi kuchukua hatua dhidi ya maafisa wa jeshi la polisi wanaohusika na vitendo vya kikatili dhidi ya wanawake wagombea ili iwe fundisho kwa wote wenye dhamana ya kulinda utu na haki za binadamu hususani haki za Wanawake kama zilivoainishwa kwenye Katiba (Ibara 12-29).

Pia tunataka yafuatayo yafanyike :-

1. Wagombea na makada wa vyama vya siasa hususani wanaume kuacha mara moja kudhalilisha wanawake wagombea kwa kuwapiga au kuwatolea lugha chafu zenye maneno ya kudhalilisha na kutweza utu wa mwanamke na msichana.

2. Kuheshimu utu na usawa wa kijinsia bila ubaguzi wa rangi ama itikadi za mgombea.

3. Tume za uchunguzi na ofisi ya msajili wa vyama vya siasa pamoja na jeshi la polisi kuhakikisha kunakuwepo na mazingira salama kwa wanawake kufurahia haki yao ya kushiriki kupiga kura na kuchagua viongozi wanaowataka.

4. Vyombo vya dola, taasisi mbalimbali vifanye kazi kwa kuzingatia matakwa ya Katiba na sheria za nchi.

5. Serikali na taasisi zake ina wajibu wa kusimamia umoja wa kitaifa ili kuendelea kulinda amani ya nchi na haki za binadamu.

6. Taasisi za dini kusimama katika nafasi na kukemea vitendo hivi viovu na vya kudhalilisha wanawake.

7. Vyama vya siasa kwa pamoja kupinga vitendo hivi vya kikatili dhidi ya wanawake wagombea pamoja na wapiga kura.

8. Wanawake wa vyama vya siasa kuungana na kuleta nguvu ya pamoja kupigania nafasi za uongozi za wanawake ili kuleta usawa wa kijinsia katika ngazi za maamuzi kwa maendeleo ya Taifa.

9. Wanawake wa Tanzania kwa ujumla kuungana na kukataa udhalilishaji wa wanawake popote unapojitokeza bila kusubiri taasisi au mamlaka kuwasemea.

10. Wanajamii kwa ujumla kupaza sauti bila woga kukemea vitendo vyote vya ukatili dhidi ya mtu yeyote.

Mwisho, sisi Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu tunatoa pole kwa wanawake wagombea waliokutana na kadhia za udhalilishaji na ukatili. Tunaamini wanawake tunaweza kuleta mageuzi na kukataa mifumo dhalilishi. Tunaamini binadamu wote ni sawa licha ya tofauti zetu za kiitikadi, dini, jinsi au rangi ya mtu.

Tuendelee kudumisha amani ya Tanzania, kuna maisha baada ya Uchaguzi.

**Imetolewa Oktoba 16, 2020 na**

**Mtandao wa Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu.**